# Mfumo Wetu wa Kutoboa Siri

## KWA MUHTASARI

Ulinzi | Haki | Uaminifu

Kutii kanuni za kisheria na kanuni za ndani na kanuni zilizobainishwa katika Kanuni zetu za Maadili Mema na Kanuni za Maadili Mema kwa Washirika wa Kibiashara, ni masuala yanayopewa kipaumbele zaidi katika kampuni ya **Volkswagen Mobility Solutions Rwanda.** Ni muhimu kutambua uwezekano wa kutekelezwa kwa mwenendo usiofaa na mfanyakazi au muuzaji na kuukomesha. Kwa hivyo, tulikabidhi Ofisi Kuu ya Upelelezi uwezo wa kuendesha Mfumo wa Kutoboa Siri ambao ni huru, wa haki na wa siri kwa niaba yetu. Kulingana na kanuni za kutoa maamuzi ya haki, Mfumo huu wa Kutoboa Siri unahakikisha ulinzi wa juu zaidi iwezekanavyo kwa watoboa siri, watu walioripotiwa na wafanyakazi wanaochangia kwa upelelezi wa mwenendo usiofaa ulioripotiwa.

Ikiwa ripoti yako inahusu uwezekano wa wauzaji kutekeleza makosa makubwa ya ukiukaji wa kanuni zinazohusiana na haki za binadamu na mazingira, Ofisi ya Upelelezi itafahamisha idara zinazohusika, ambazo zitashughulikia suala hilo ipasavyo.

Pata maelezo zaidi kuhusu kanuni za jumla za Utaratibu wa Kuwasilisha Malalamiko za Volkswagen Group hapa.

**Kuwasilisha ripoti kwa Mfumo wetu wa Kutoboa Siri**

Mfumo wa Kutoboa Siri unatoa njia mbalimbali za kuripoti uwezekano wa kutekelezwa kwa mwenendo usiofaa na mfanyakazi na muuzaji ambazo zinawezesha kampuni yetu kuchunguza na kuchukua hatua haraka ikiwa inahitajika. Ripoti zinaweza kuwasilishwa wakati wowote usiku na mchana, kila siku ya wiki.

**Ana kwa Ana**
Weka miadi kupitia barua pepe kabla ya kutembelea ofisi

**Anwani ya posta**
Volkswagen AG – Central Investigation Office, Mailbox 1717, Berliner Ring 2, 38436 Wolfsburg (Ujerumani)

**Anwani ya Barua Pepe**
io@volkswagen.de

**Njia ya kuripoti ya mtandaoni**
https://goto.speakup.report/volkswagen

**Wachunguzi Maalum**
http://www.ombudsmen-of-volkswagen.com

24/7
**Kuwasilisha Ripoti kwa Matamshi kupitia Simu**
Namba ya simu: +254 20 765 0957
(utatozwa ada za kawaida za kupiga simu)
Namba ya shirika: 122203

**Programu**
**Hatua ya 1:** Pakua Programu kwa kutumia msimbo wa QR ambao ni:

**Hatua ya 2:** Weka namba ya Shirika: **122203** au changanua msimbo wa QR ambao ni:

**Una maswali zaidi?**

Tafadhali elekeza maswali au mapendekezo ya uboreshaji wa Mfumo wa Kutoboa Siri kwa Ofisi ya Upelelezi.



INTERNAL